HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO

Barua pepe:info@nsimbodc.go.tz
Tovuti:www.nsimbodc.go.tz

S.L.P 688

MPANDA

Press No: NDC/ICPRU/Press no.23 **18 Agusti 2018**

TAARIFA KWA UMMA/VYOMBO VYA HABARI

YALIYOJIRI KATIKA KIKAO CHA MKURUGENZI MPYA WA HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO BW.RAMADHANI MOHAMMED NA WAKUU WA IDARA NA VITENGO MARA BAADA YA KURIPOTI AGOSTI 17, 2018 KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo **Bw.Ramadhani Mohammed** ameripoti rasmi katika kituo chake kipya cha kazi tayari kuanza utekelezaji wa majukumu yake tangu kuteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr.John Pombe Joseph Magufuli.Agosti 13, 2018.

Bw.Mohammed aliwasili Nsimbo **Agosti 17** na kupokelewa na **Bw.Betuely Ruhega** ambaye ni Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala aliyekaimu nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji kufuatia aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji **Bw.Mwailwa Pangani** kuhamishiwa Manispaa ya Kigoma.

Akiwa kituo kipya cha kazi Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo Mkurugenzi Mtendaji **Bw.Ramadhani Mohammed** alianza kazi mara moja kwa kukutana na kufanya mazungumzo kwa nyakati tofauti na Wakuu wa Shule,Maafisa Elimu Kata pamoja na wakuu wa Idara na Vitengo katika Ukumbi wa Halmashauri.

Akizungumza na Wakuu wa Idara na Vitengo majira ya saa Tisa Alasiri ikiwa ni masaa machache baaada ya kuripoti Nsimbo Mkurugenzi **Ramadhani Mohammed** amewataka Wakuu hao wa Idara na Vitengo kujitambua na kutekeleza majukumu yao kikamilifu ili kutimiza adhma kubwa ya Serikali ya kuhakikisha kuwa **Wananchi wanapata huduma bora na za kuridhisha.**

Amesema iwapo Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri watasimamia kikamilifu majukumu ya kiutendaji ndani ya Idara zao na Vitengo ,pamoja na kusimamia kikamilifu watumishi walio chini yao, itachochea kwa kiasi kikubwa **kasi ya Utendaji kazi** jambo litakaloondoa kwa sehemu kubwa **Urasimu katika utoaji Huduma kwa Wananchi.**

Amewataka wakuu wa Idara na Vitengo Nsimbo **kuepuka kufanya kazi kimazoea** na badala yake kufanya kazi kwa bidii na kwa kuzingatia **Mpango kazi wa Idara au Kitengo** ili kuendana na kasi ya Utendaji kazi ya Serikali ya awamu ya tano.

Bw.Mohammed ameeleza kukerwa na tabia ya baadhi ya wakuu wa Idara na Vitengo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hususani Halmashauri kutotekeleza majukumu yao kimamilifu kwa kutoa visingizio vingi ikiwemo **kukosa Posho** ilhali zipo njia mbadala zinazoweza kutumika kufanikisha utekelezaji wa shughuli husika.

*"Sio shughuli zote za Idara zinahitaji fedha katika utekelezaji wake,nyingine zinahitaji tu Mkuu wa Idara, kitengo ama Mtaalamu husika kutumia njia mbadala na shughuli husika ikatekelezeka"*alisisitiza Mkurugenzi Mohammed.

Amesema kutokana na changamoto ya uhaba wa fedha tatizo linalozikabili Halmashauri nyingi Nchini, ni vema Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ya Nsimbo na kote Nchini wakawa wabunifu na kujikita katika **kutumia njia mbadala** za utekelezaji wa baadhi ya shughuli zao badala ya kuendekeza visingizio ikiwemo kisingizio cha kukosa Posho jambo linaloathiri kasi ya Utendajji kazi ya awamu ya tano na kupelekea Wananchi kutopata huduma kwa wakati.

Aidha amewataka Wakuu wa Idara na Vitengo Nsimbo kusimamia kikamilifu watumishi wa Idara na Vitengo walioko Chini yao ili kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kikamilifu, sambamba na **kuhakikisha Ujazaji wa Fomu za OPRASS** kwa wakati zitakazotumika kupima utendaji kazi wa watumishi hao.

Amewetaka Wakuu wa Idara na Vitengo Nsimbo kwa kushirikiana na wataalamu wao kuhakikisha **wanajibu kwa wakati barua zinazohusu maagizo yanayotolewa na mamlaka za juu,na taasisi zingine** ili kuharakisha utekelezaji wa shughuli husika licha ya kuwepo kwa changamoto ya kosefu wa miundombinu ya kisasa ya mawasiliano.

Mkurugenzi pya wa Nsimbo amezungumzia pia umuhimu wa Watumishi wa Makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kuhakikisha wanatumia fursa ya **Viwanja vilivyopimwa katika Halmashauri hiyo kusogea na kuishi karibu na Ofisi jambo litakaloboresha utoaji huduma bora kwa Wananchi kwa wakati.**

Bw.Mohammed amebaini kitendo cha Watumishi wengi wa Makao makuu ya Halmashauri ya Nsimbo na baadhi ya Vituo kutoishi katika maeneo ya karibu na Ofisi zao na kusema kuwa jambo hilo, huathiri kwa kiasi kikubwa mahudhurio ya Watumishi kazini jambo linalopelekea shughuli nyingi kutokukamilika kwa wakati na hivyo kuathiri utoaji huduma bora kwa Wananchi.

Mbali na maagizo muhimu aliyoyatoa,**Mkurugenzi Ramadhani Mohammed** amewaomba wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na watumishi kwa ujumla, kumpa **ushirikiano wa kutosha ili kwa pamoja waweze kutekeleza adhma ya Serikali** ya utoaji huduma kwa wakati ,ubora na viwango vinavyotakiwa na hivyo kutekeleza adhma ya Serikali ya awamu ya tano ya Utoaji huduma bora kwa Wananchi na kuharakisha Maendeleo.

Imetolewa na:

John A. Mganga

Afisa Habari Mawasiliano na Uhusiano(W)
Kitengo cha Habari Mawasiliano TEHAMA na Uhusiano
Ofisi ya Mkurugernzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo.